



CROWN EXAMINATION TEST

MONITORING LEARNER'S PROGRESS

GREDI 2 - MUHULA WA TATU - 2021

SHUGHULI ZA KISWAHILI

Jina: _____

Shule: _____

VIWANGO VYA KUTATHMINI

Kuzidisha Matarajio	Kufikia Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali na Matarajio

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

(Alama 5)

1. Mzazi wako anaitwa aje?

_____.

2. Uko na umri wa miaka ngapi?

_____.

3. Ni mnyama gani mnafuga nyumbani?

_____.

4. Ni siku gani unaenda kuomba?

_____.

5. Wewe ni msichana ama mvulana?

_____.

KUSOMA KWA SAUTI (Alama 15)

Soma sentensi zifuatazo kwa sauti.

1. mama anaenda sokoni

2. Mwalimu anaandika ubaoni

3. Baba analima shambani

4. Chakula kitamu kinapikwa

5. Kuna mawingu angani

SARUFI (Alama 20)

1. Andika sentensi zifuatazo kwa wingi

(Alama 5)

(a) Kitabu chako - _____

(b) Kalamu yako - _____

(c) Mtoto wako - _____

(d) Jino lako - _____

(e) Darasa lako - _____

2. Kanusha maneno. (Alama 5)

(a) Kimbia - _____

(b) Soma - _____

(c) Kuja - _____

(d) Imba - _____

(e) Cheka - _____

3. Andika kinyume. (Alama 5)

- (a) Lala
- (b) Enda
- (c) Lia
- (d) Simama
- (e) Jenga

4. Jibu maamkuzi. (Alama 5)

- (a) Shikamoo?
- (b) Hujambo?
- (c) Habari?
- (d) Umeshindaje?
- (e) Hamjambo?

UFAHAMU (Alama 5)

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali.

Kuna wanyama wengi wanaofugwa nyumbani. Hawa wanyama hutupatia faida nyingi.

Kuku hutupatia mayai na nyama. Nyama ya kuku ni tamu sana. Watoto wanapenda sana mayai. Mbuzi hutupatia maziwa na nyama. Ng'ombe pia hutupatia maziwa na nyama. Kondoo naye hutupatia nyama na manyoya. Manyoya hutumika kutengeneza nguo ambazo tunavaaa.

Mbwa naye hulinda nyumbani kwetu.

Maswali.

1. Taja aina mbili ya wanyama wanaofugwa nyumbani.

2. Ni mnyama gani hulinda nyumbani kwetu?

3. Taja wanyama wawili ambaa hutupea maziwa na nyama.

4. Taja mnyama ambaye hutupea nyama na mayai

5. Manyoya hutumika kutengeneza nini?

KUANDIKA (Alama 10)

Andika sentensi tano kuhusu shule yenu
